

TANGAZO LA SERIKALI Na. 12 la tarehe 3/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),  
SURA YA 287

---

**SHERIA NDOGO**

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MASOKO YA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE YA  
MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Masoko ya Halmashauri ya Wilaya ya Mji Njombe ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Mji Njombe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-  
“afisa mwidhiniwa” maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;  
“bidhaa” maana yake ni mazao, mifugo au kitu chochote chenye thamani kinachopelekwa sokoni kwa ajili ya kuuzwa;  
“dalali” maana yake ni mtu anayeenza bidhaa sokoni kwa njia ya mnada kwa niaba ya mwenye bidhaa;  
“gulio” maana yake ni soko la wazi linalofanyika kwa wakati maalumu kwa kibali cha Halmashauri;  
“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Mji Njombe;  
“kibali” maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

- “kikundi” maana yake ni kikundi cha ushirika wa wafanyabiashara kilichosajiliwa au kuandikishwa au umoja wa vikundi vyawafanyabiashara uliosajiliwa au kuandikishwa na kutambuliwa na Kamati ya Wadau wa Soko na Halmashauri;
- “makasha” maana yake ni vifaa maalumu vya kubebea, kufungashia au kuhifadhia bidhaa na inajumuisha matenga, viroba, magunia, karatasi ngumu, majani, masanduku ya mbao kitu kingine chenye matumizi hayo;
- “masoko” inajumuisha mnada na gulio;
- “mazao” maana yake ni mavuno ya shambani au maliasili yanayoingizwa sokoni;
- “meneja wa soko” maana yake ni mtu aliyeteuliwa au aliyeajiriwa na Halmashauri kwa ajili ya kusimamia shughuli zote katika soko;
- “meza au kizimba” maana yake ni kitu au kifaa kinachotumika kuweka bidhaa kwa ajili ya kuuza katika soko;
- “mfanyabiashara” maana yake ni mtu anayeenza bidhaa sokoni kwa jumla au rejareja;
- “Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au afisa atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;
- “mnada” maana yake ni soko la wazi lililoidhinishwa na Halmashauri ambalo bidhaa huuzwa kwa ushindani wa bei;
- “soko” maana yake ni eneo maalumu la biashara lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa;
- “wadau wa soko” maana yake ni wafanyabiashara binafsi au vikundi vinavyofanya shughuli za biashara katika soko;
- “wakala” maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoingia mkataba kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa  
Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

- (a) kuanzisha, kusimamia na kuboresha miundombinu ya masoko;
- (b) kuendeleza masoko;
- (c) kusimamia afya na usafi wa masoko;
- (d) kudumisha usalama wa masoko kwa kuweka utaratibu mzuri wa ulinzi;
- (e) kutoa na kusimamia huduma za kijamii katika masoko;
- (f) kugawa na kupangisha vyumba, vibanda, meza au vizimba katika masoko;
- (g) kutenga maeneo kwa ajili ya minada na magulio;
- (h) kukusanya ushuru au ada kutoka kwa wafanyabiashara wa masoko;
- (i) kusajili wafanyabiashara katika masoko; na
- (j) kukagua masoko binafsi kwa madhumuni ya kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Halmashauri.

Meneja wa soko

5.-(1) Kutakuwa na meneja wa soko atakayeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kusimamia shughuli za uendeshaji wa soko.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), meneja wa soko-

- (a) atasimamia ukusanyaji wa ushuru na ada;
- (b) atasimamia usajili wa wadau wa soko kwa kushirikiana na kamati ya wadau wa soko;
- (c) ataimarisha huduma za ulinzi, maji na umeme katika soko;
- (d) atasimamia usafi na uondoshaji wa taka katika soko;
- (e) atahakikisha kuwa bidhaa haziuzwi kwenye eneo ambalo haliruhusiwi kwa shughuli hiyo;
- (f) atazuia ujenzi holela katika soko; na
- (g) atatekeleza majukumu mengine atakayoagizwa na Halmashauri.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kuingia mkataba na wakala kwa

ajili ya kusimamia au kushughulikia majukumu mahsusi ya uendeshaji wa soko kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala.

Kamati ya  
Wadau wa Soko

6.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Wadau wa Soko ambayo itaundwa na wadau wa soko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Kila kikundi katika soko kitakuwa na mwakilishi mmoja katika Kamati ya Wadau wa Soko.

(3) Kamati ya Wadau wa Soko itaandaa na kuwasilisha Halmashauri utaratibu maalumu wa-

(a) kuwapata viongozi;

(b) kuondoa viongozi madarakani; na

(c) uendeshaji wa shughuli za Kamati ya Wadau wa Soko.

(4) Vikao vya Kamati ya Wadau wa Soko vitafanyika angalau mara moja kila mwezi.

(5) Meneja wa soko atakuwa katibu katika kikao cha Kamati ya Wadau wa Soko.

(6) Muda wa wajumbe wa Kamati ya Wadau wa Soko kuwa madarakani ni miaka mitatu.

Majukumu ya  
Kamati ya  
Wadau wa Soko

7. Kamati ya Wadau wa Soko itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuhakiki aina za biashara zinazoendeshwa katika soko;

(b) kuboresha ustawi wa wadau wa soko;

(c) kusimamia nidhamu katika shughuli za soko;

(d) kuhakikisha wadau wa soko wanalipa ushuru au ada;

(e) kukuza na kuendeleza mfumo wa biashara;

(f) kuhakikisha kila eneo la mdau wa soko linakuwa safi muda wote;

(g) kuratibu mipango ya kugharamia huduma za ulinzi, usafi, maji na umeme katika soko;

(h) kusimamia usajili wa wadau wa soko kwa kushirikiana na meneja wa soko; na

(i) kutekeleza kazi nyingine watakazoelekezwa na Meneja wa soko kulingana na Sheria Ndogo hii.

Kamati ndogo

**8.-(1)** Kamati ya wadau wa soko itaunda kamati ndogo zenye wajumbe wanne kutoka miongoni mwa wajumbe wa kamati ya wadau wa soko ambazo zitajumuisha-

- (a) kamati ndogo ya miundombinu na safi;
- (b) kamati ndogo ya utawala na biashara; na
- (c) kamati ndogo ya ulinzi na usalama.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), kamati ya wadau wa soko inaweza kuunda kamati ndogo nyingine kadiri itakavyohitajika.

Usajili wa wadau

**9.** Mtu anayekusudia kufanya biashara katika eneo la soko atatakiwa kusajiliwa na meneja wa soko akishirikiana na kamati ya wadau wa soko kwa ajili ya utambuzi na kuandikishwa katika rejesta ya wadau wa soko.

Wajibu wa mfanyabiashara

**10.** Kila mfanyabiashara katika eneo la soko atakuwa na wajibu ufuatao:

- (a) kujiandikisha katika rejesta ya wadau wa soko;
- (b) kulinda na kuhifadhi miundombinu ya soko;
- (c) kufanya biashara katika maeneo yanayoruhusiwa;
- (d) kufanya usafi katika eneo analofanyia biashara;
- (e) kulipa ushuru au ada kwa wakati;
- (f) kutobandika au kutobandua tangazo bila idhini ya meneja wa soko;
- (g) kushiriki usafi wa jumla wa soko;
- (h) kutotupa taka ovyo au kutiririsha maji machafu;
- (i) kutowasha moto maeneo yasiyohusika ndani ya soko;
- (j) kuzingatia miongozo itakayotolewa na viongozi wa soko; na
- (k) kuzingatia masharti ya upangaji.

Muda wa  
biashara

**11.-(1)** Soko litakuwa wazi siku ya Jumatatu hadi Jumapili.

(2) Mkurugenzi kwa kushauriana na meneja wa soko, anaweza kufunga soko kwa ajili ya matengenezo au sababu nyingine yoyote ya dharura iwapo itaonekana inafaa, isipokuwa kwamba Mkurugenzi atatoa notisi ya siku saba kwa wadau wa soko kuhusu kusudio la kufunga soko kwa ajili ya matengenezo.

Ada ya  
kupangisha

**12.-(1)** Kila mfanyabishara katika soko atalipa ada ya kupangisha chumba, kibanda, meza au kizimba kwa mujibu wa mkataba.

(2) Halmashauri inaweza kwa makubaliano maalumu kumruhusu mtu kujenga chumba au kibanda cha biashara katika soko.

Ada na ushuru  
wa masoko

**13.** Halmashauri itatoza ada na ushuru wa soko kutoka kwa kila mfanyabiashara aliyesajiliwa kufanya biashara katika eneo la masoko kwa viwango na utaratibu ulioainishwa kwenye sheria ndogo ya ada na ushuru iliyotengenezwa na Halmashauri ya Mji Njombe.

Kibali cha soko  
kwa muda

**14.-(1)** Mfanyabiashara ambaye hakuandikishwa katika rejesta ya wadau wa soko anaweza kutumia soko kwa muda kwa kibali maalumu cha kutumia soko kwa muda.

(2) Maombi ya kibali cha kutumia soko kwa muda yatawasilishwa kwa Mkurugenzi kwa kutumia fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kibali cha  
minada na  
magulio

**15.-(1)** Minada na magulio inaweza kufanyika kwa kibali maalum cha Halmashauri.

(2) Minada na magulio itafanyika katika muda na maeneo maalumu yatakayotengwa na Halmashauri.

(3) Minada na magulio itasimamiwa na afisa mwidhiniwa.

Uendeshaji wa  
minada

**16.-(1)** Bidhaa itakayoingizwa katika soko kwa ajili ya kuuzwa kwa mnada itapokelewa na dalali

atakayeteuliwa na wafanyabiashara na kukubaliwa na kamati ya wadau wa soko.

(2) Dalali atauza bidhaa husika katika eneo lililotengwa kwa shughuli hiyo.

Mifugo  
isiyoruhusiwa  
ndani ya soko

**17.** Mfanyabiashara hataruhusiwa kuingiza mifugo ndani ya soko isipokuwa mifugo ya jamii ya ndege na wanyama wadogo kama sungura.

Ufungaji wa  
bidhaa

**18.-(1)** Mfanyabiashara anayeingiza bidhaa katika masoko inayopaswa kufungashwa atafungasha bidhaa hizo kwenye makasha.

(2) Mfanyabiashara atapaswa kuondoa makasha katika eneo la soko kwa gharama zake baada ya bidhaa kuondolewa kwenye makasha.

Makosa

**19.** Mtu anatenda kosa endapo-

- (a) atabandika au atabandua tangazo bila idhini ya meneja wa soko au afisa mwidhiniwa;
- (b) atafanya shughuli yoyote inayohusisha matumizi ya moto bila idhini ya maandishi ya meneja wa soko;
- (c) atatembeza bidhaa ndani ya soko bila kibali;
- (d) atafanya shughuli yeyote kwenye eneo ambalo haliruhusiwi au halijatengwa kwa shughuli hiyo;
- (e) ataharibu miundombinu ya masoko;
- (f) atafanya ujenzi au ukarabati bila kibali;
- (g) atatupa taka ovyo au kutiririsha maji machafu; au
- (h)kutolipa ada na ushuru wa masoko.

Adhabu

**20.** Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyo pungua shilingi elfu hamsini na isiyo zidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita jela na kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.

Kufililisha kosa

**21.** Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa kwa kumtoa mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

Kufutwa kwa  
Sheria Ndogo  
TS. Na.  
127 la 2008

**22.** Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko ya Halmashauri ya Mji Njombe inafutwa.



JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15(1) na (2))*

KIBALI CHA KUTUMIA SOKO KWA MUDA

1. Jina la Mwombaji .....
2. Anuani ya Mwombaji .....
3. Matumizi yanayokusudiwa .....
4. Eneo maalum la Soko linalokusudiwa kutumiwa (Kama ni muhimu kutaja)  
.....
5. Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni kweli na niko tayari kuzingatia masharti ya kibali iwapo nitapewa kibali.

Jina la Mwombaji .....

Saini .....

Tarehe .....

6. Kibali hiki hakitahamishika.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Namba ya kibali ..... Tarehe.....,Mahali .....

Stakabadhi Na. ....ya Tarehe.....

Jina: .....

Saini:.....

Wadhifa:.....

Muhuri:.....

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 21)*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi.....NAKIRI KWA HIARI YANGU  
MWENYEWE mbele ya ..... ambaye ni Mkurugenzi wa  
Halmashauri ya Wilaya ya ....., kwamba mnamo tarehe ..... ya mwezi ..... Mwaka .....  
nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya ..... ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Masoko  
ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ya Mwaka 2024.

NAKUBALI kulipa ada ninayodaiwa ya kiasi cha shilingi ..... pamoja na faini ya  
kufifilisha kosa ya kiasi cha shilingi .....

NATHIBITISHA KWAMBA, maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa MIMI  
MWENYEWE na kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo hii tarehe.....ya mwezi..... mwaka 20.....

Jina.....

Saini.....

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:.....

Saini:.....

Tarehe:.....

Lakiri ya Halmashauri ya Mji wa Njombe imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azinio lililopitishwa katika Mkutano wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Njombe uliofanyika tarehe 3/5/2023:-

KURUTHUM A. SADICK,  
*Mkurugenzi,*  
*Halmashauri ya Mji,*  
*Njombe*

ERASTO B. MPETE,  
*Mwenyekiti,*  
*Halmashauri ya Mji,*  
*Njombe*



NAKUBALI,

Dodoma,  
29 Agosti, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,  
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*